

MASWALI YANAYOULIZWA MARA KWA MARA (FAQs)

KUHUSIANA NA NOTISI ILIYOCHEPISHWA KATIKA GAZETI RASMI LA SERIKALI KUHUSU MARUFUKU YA KUTUMIA, KUTENGENEZA NA KUAGIZA KUTOKA NJE MIFUKO YA PLASTIKI.

SWALI 1: Ni Mifuko ipi ya plastiki imepigwa marufuku?

JIBU: Marufuku hiyo inahusisha mifuko yote ya plastiki inayotumika kubebaa au karatasi nyembamba za kufungia bidhaa za kibiashara au nyumbani.

SWALI 2: Mfuko wa plastiki wa kubebaa bidhaa ukoje?

JIBU: Hii ni mifuko ya plastiki inayoweza kutumika mara moja na ina sehemu ya kushikia juu. Inaweza kuwa na sehemu ya ndani au la.

SWALI 3: Karatasi za plastiki nyembamba ni ipi?

JIBU: Huu ni mifuko usiokuwa na sehemu ya juu ya kushikia na unaweza kuwa na sehemu ya ndani au la.

SWALI 4: Nini kilichosababisha mifuko ya plastiki kupigwa marufuku?

JIBU: Kwa kawaida mifuko ya plastiki hutengenezwa kwa ajili ya matumizi ya mara moja tu na kisha kuharibika na kutupwa baada ya kutumika. Mifuko hiyo inapeperushwa na upopo kwa urahisi na miiongoni mwa takataka zilizorundikana kando ya barabara, kingo za mito, fukwe za maziwa au majalalani. Mifuko ya plastiki inatengenezwa kutokana na mafuta na gesi za kiasili, hivyo haziozi na husalia ardhini kwa muda mrefu zinapofukiwa.

SWALI 5: Je, mifuko ya plastiki inayotumiwa viwandani kufunga bidhaa pia imepigwa marufuku?

JIBU: La hasha. Marufuku haijumuishi mifuko inayotumiwa viwandani kufunga bidhaa, almradi iwe imetimiza viwango vya ubora vilivyowekwa.

SWALI 6: Je, siku ya mwisho ambayo watengenezaji na waagizaji wa bidhaa wanafaa kukoma kuwapa wateja wao mifuko ya plastiki ni ipi?

JIBU: Makataa ya kuwapa wateja mifuko ya plastiki ni Agosti 28, 2017. Baada ya makataa, watengenezaji na waagizaji wa bidhaa wanastahili kuripoti kwa Mamlaka ya Usimamizi wa Mazingira (NEMA) kuhusu kiasi cha karatasi zilizosalia bila kutumika ili hatua madhubuti zichukuliwe.

SWALI 7: Je, viwanda vinavyotengeneza mifuko ya plastiki ya kuza nje ya nchi vitaendelea kuitenegeneza?

JIBU: La hasha. Utengenezaji wa karatasi za plastiki utafikia kikomo Agosti 28, 2017.

SWALI 8: Je, kutakuwa na muda zaidi wa kipindi cha neema kwa wafanyabiashara kuanza kutekeleza marufuku hiyo?

JIBU: Notisi katika Gazeti Rasmi la Serikali ilichapishwa mnamo Februari 28, 2017 kwa lengo la kuruhusu kipindi cha neema cha miezi sita (6) kabla ya kuanza kutekelezwa Agosti 28, 2017.

SWALI 9: Je, wafanyabiashara na wenyewe maduka wataruhusiwa kuendelea kutumia mifuko ya plastiki watakayosalia nayo baada ya makataa ya Agosti 28, 2017?

JIBU: Hapana. Wafanyabiashara, wakiwemo wenyewe maduka, wanastahili kutumia mifuko yote ya plastiki iliyosalia katika kipindi hiki cha neema kabla ya makataa. Baada ya makataa, wenyewe maduka na wafanyabiashara wengineo watatakiwa kuwasilisha ripoti kwa NEMA kuhusiana namifuko iliyosalia ili hatua mwafaka zichukuliwe.

SWALI 10: Je, wafanyabiashara wanaweza kutumia mifuko ya karatasi za kawaida badala ya mifuko ya plastiki kuwafungia wateja bidhaa?

JIBU: Ndiyo.

SWALI 11: Je, ni mifuko ipi ya karatasi za kawaida inayofaa kutumiwa badala ya mifuko ya plastiki?

JIBU: Mifuko mbadala inajumuisha, mifuko iliyotengenezwa kwa karatasi za kawaida, nguo, vikapu, mifuko iliyotengenezwa kwa nyuzi za mikonge na mifuko na begi wanazokuja nazo wateja.

SWALI 12: Ni maduka yapi yameathiriwa na marufuku hiyo?

JIBU: Maduka na wafanyabiashara wote.

SWALI 13: Je, Wafanyabiashara wadogo wanaouza bidhaa za rejareja wanaruhusiwa kutumia karatasi za plastiki?

JIBU: La hasha.

SWALI 14: Je, marufuku hiyo inazuia uuza wa karatasi za plastiki zinazotumika kubebaa takataka?

JIBU: Ndiyo.

SWALI: Je, maduka ya kuuza nguo yameruhusiwa kutumia mifuko ya plastiki baada ya makataa?

JIBU: Hapana. Wanaoruhusiwa kutumia karatasi hizo ni viwanda vya kutengeneza bidhaa ambavyo ni sharti vitumie karatasi zilizoidhinishwa kama ilivyoolezwa katika swali la tano (5).